


RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA YA MWEZI AGOSTI 2026

BONDE LA MTO WAMI


1.0 MTIRIRIKO WA MAJI KATIKA MTO WAMI

Katika kituo cha Wami/Mandera (1G2), wastani wa mtiririko wa maji mwezi Agosti 2026 ulikuwa **9.395 m³/s** ambao ni chini ya wastani wa muda mrefu wa **11.92 m³/s**, lakini juu ya **7.66 m³/s** ya Agosti 2025. Kupungua kwa mtiririko ikilinganishwa na **Julai 2026** kulitokana na uhaba wa mvua katika maeneo ya vyanzo, hususan Milima ya Nguu na Ukaguru pamoja na Mkoa wa Dodoma na Manyara.




Aidha, katika kituo cha Wami/Dakawa (1G1), wastani wa mtiririko wa maji uliorekodiwa Agosti 2026 ulikuwa **17.24 m³/s**, kiwango ambacho ni juu ukilinganisha na wastani wa muda mrefu wa **13.71 m³/s** na pia juu ya **9.27 m³/s** kilichorekodiwa Julai 2025.

Na. ya Kituo	Agosti 2026 (m ³ /s)	Agosti 2025 (m ³ /s)	Wastani wa Muda Mrefu (2000-2025)	Mahitaji (m ³ /s)
1G1	13.46	7.015	5.43	2.3
1G2	9.395	7.66	11.92	5.5




2.0 RAMANI YA VITUO NA MITO INAYOLISHA MTO WAMI




3.0 HALI YA MVUA

Mwezi Agosti 2026 Bonde la Mto Wami liliopokea mvua chini ya wastani ukilinganisha wastani wa muda mrefu (1995–2025) sawa na Mwezi Julai 2025, ambapo vituo vingi vilirekodi kati ya 0–5 mm pekee. Kiwango cha juu kimerekodiwa katika Kituo cha Murad saddiq kikiwa na mvua kiasi cha **28.6 mm**. Upungufu huu wa mvua ulisababisha kupungua kwa mtiririko wa maji, lakini kiwango kilichopo katika hifadhi ya maji makutupora bado kinatosha na kitaendelea kukidhi mahitaji.



4.0 UTABIRI WA MVUA MWEZI JUNI

Kwa mujibu wa utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mwezi Septemba 2026 katika Bonde la Wami/Ruvu unatarajiwa kuwa na mvua nyepesi hadi mvua, huku baadhi ya maeneo yakitarajiwa kuwa na vipindi vya ukavu. Mvua hiyo inatarajiwa kujitokeza katika wiki zote za mwezi, kwa viwango vinavyotofautiana kulingana na maeneo. Hali hii inaweza kusaidia kuongeza kwa kiwango kidogo upatikanaji wa maji katika mito na vyanzo vya maji katika Bonde..



5.0 MAPENDEKEZO

Mwezi Septemba 2026, rasilimali za maji zinatarajiwa kupungua kutokana na vipindi vya ukavu katika baadhi ya maeneo, sambamba na mvua nyepesi hadi mvua katika wiki tatu za mwanzo na mvua nyepesi wiki ya nne. Wadau wanashauriwa kutumia maji kwa ufanisi na kulinda vyanzo vya maji ili kukabiliana na ukavu vinavyotarajiwa.

ANGALIZO: Pamoja na ukame unaotarajiwa, wadau wanapaswa kuwa na tahadhari juu ya uwezekano wa mvua za El Niño kuanza katika maeneo mbalimbali kuanzia mwezi Oktoba 2026.



Imetolewa tarehe 31 Agosti, 2026
Na: Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu